Toleo 52 - Ramadhan 1442 AH / Mei 2021 M

Jarida la

# UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Ramadhani Inaingia huku Umma ukiendelea kukumbwa na maafa zaidi

**HABARI NA MAONI**
BATUK - Zana ya Kikoloni yenye Kulinda Maslahi na Ajenda ya Kikoloni

**TOLEO JIPYA**
Ramadhan: Tuzidisheni Juhudi Katika Ulinganizi wa Kurudisha Khilafah

**JIBU LA SWALI**
Tofauti ya Rai za Kifiqhi Kwa Mfano Kuthubutu Kuanza kwa Kufunga Ramadhan



Afisi ya Habari
ya Hizb ut Tahrir
Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 10/1442 Jumamosi, 28 Sha'aban 1442 H 10/04/2020 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Ramadhani Inaingia huku Umma ukiendelea kukumbwa na maafa zaidi

Harakati ya Hizb ut-Tahrir Kenya inafuraha kupongeza Waislamu humu nchini na kote duniani kwa ujumla kwa kufikiwa na Mwezi mtukufu wa Ramadhan. Tunapoingia kwenye mwezi huu wa rehema, msamaha na kuachwa huru na Moto, tungependa kuwakumbusha Waislamu waweze kuisoma Quran kwa wingi wakitafakari maana yake kwa lengo la kujifunga na mafundisho yake.

Ramadhani inaingia huku baadhi ya maeneo yakiwemo mji mkuu wa Nairobi yapo kwenye marufuku ya kutembea usiku na kuingia au kutoka katika kile kiitwacho kupambana na msambao wa Corona, hali inayohujumu uchumi wa wakenya wengi. Isitoshe, kwa hatua hiyo kaka na dada zetu wa Kiislamu wa maeneo hayo hawatoweza kutekeleza swala za Jamaa katika kipindi kizima cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Tunabaini kwamba hatua ya kuweka idadi maalumu ya waumini ni kinyume na Uislamu na Waislamu. Na hapa twapenda kusisitiza kuwa kwenye kipindi cha maradhi ya maambukizi, sheria tukufu ya Kiislamu inabaini kuwa kinachohitajika sio kufunga misikiti au kuweka idadi maalum waumini bali ni kuzuia walioambukizwa na kutengwa kutoingia Msikitini. Sambamba na haya lazima kuchukuliwe mikakati yote ya kiafya kama vile udumishaji wa usafi,uvaaji wa vitamvua, watu kupimwa na kuosha mikono.

Katika hali ya kusuasua kwa uchumi, Ramadhani inakuja huku hamu ya serikali ya ukopaji fedha kwa mataifa ya kigeni bado ingali kuwa juu. Nairobi tayari imekwisha saini mkataba na shirika la Fedha Duniani IMF kupokea kiwango cha fedha kwa muda wa miaka mitatu kama hatua ya 'kuisaidia kupambana na janga la Corona' na mpango wake wa kupunguza kiwango cha malimbikizi yake ya madeni! Ukopeshaji wa IMF na masharti yake magumu kamwe hayotoweza kuimarisha uchumi bali ni kuhujumu zaidi uchumi wa mamilioni ya wakenya. Tokea mwanzoni mwa mwaka bei za bidhaa muhimu kama unga wa ngano, maziwa, mafuta ya kupikia, mafuta taa na sukari imeongezeka juu zaidi. Sera mbaya za kiuchumi ndani ya mfumo wa Kibepari, zinazosema kwamba bei ndio kiwango cha kuamua na kutambua kasi ya uzalishaji na matumizi wa bidhaa,hali inayowafanya warasilimali kumiliki uzalishaji na usambazaji wa bidhaa. Kwa hakika hali yapaswa kuwa ukumbusho mkubwa kwamba serikali za Kibepari hazijali kabisa hali za raia wake.

Kwa yakini Ramadhani huletea Waislamu kheri lakini cha kutamausha ni kwamba hali ya Umma wa Kiislamu leo inatisha. Waislamu huko Mynmar, Syria, Filastin na Yemen bado wanakumbana na dhulma na madhila ya kila siku. Maafa haya bila shaka ni kukosekanwa kwa utekelezwaji wa Quran kwenye nyanja zote za maisha. Umma wa Kiislamu wapaswa kuelewa kwamba majanga haya yatamalizika punde tu watakapotekeleza moja wapo wa wajibu mkubwa wa Kuisimamisha tena Khilafah kwa mfumo wa Utume katika moja wapo ya mataifa makubwa ya Kiislamu. Kwa kuwa leo twaishi katika jamii ya Kisekular ya Kilibirali inayoitambua Dini kama suala la wakati na sehemu tu ya maisha,Waislamu tunalazimika kufahamu kwamba Uislamu ni mfumo kamili wa kimaisha tunapaswa kuutekeleza kikamilifu katika masuala ya kisiasa,kiuchumi na kijamii.

Mwisho twamuomba MwenyeziMungu SWT atupe nguvu kufikia kwenye lengo husika la ibada ya swaum lililotajwa kwenye Quran nalo ni uchajiMungu, nishati ya hali ya juu ya Muislamu inayomfanya aweze kujifunga na maamrisho ya MwenyeziMungu.


**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari, Hizb ut -Tahrir in Kenya**




Email: info@uqab.or.ke

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 30/1442 Jumapili, 29 Sha'aban 1442 H 11/04/2020 M

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Tangazo la Matokeo ya Kuutafuta Mwandamo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wa Mwaka 1442 Hijria

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu, na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote, Muumba wa wanadamu na Mtumaji wa manabii pamoja na risala, Mshindi wa wenye nguvu na Mtawala juu ya waja, na rehma na amani zimshukie bwana wa viumbe na mbebaji ujumbe, yule aliyetumwa na Wahyi wa kusimamisha nidhamu ya Khilafah, yule ambaye alionya juu ya kuvunjwa kwake na kutoa bishara njema za kurudi kwake, bwana wetu Muhammad na juu ya familia yake na maswahaba zake wote.

Al-Bukhari amepokea katika Sahih yake kutoka kwa Muhammad bin Ziyad, aliyesema: Nilimsikia Abu Hurairah, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe pamoja naye, amesema: Mtume (saw) amesema, au alisema Abu Al-Qasim (saw) amesema,

«صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَأَكْمِلُوا عِدَّةَ شَعْبَانَ ثَلَاثِينَ»

**"Fungeni kwa kuonekana kwake (mwandamo wa mwezi wa Ramadhan), na fungueni kwa kuonekana kwake (mwandamo wa mwezi wa Shawwal), na ikiwa mawingu yametanda juu yenu (kiasi cha kutouona) basi kamilisheni hesabu ya (siku) thalathini za Sha'aban."**

Baada ya kuutafuta mwandamo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan usiku huu, mkesha wa Jumatatu, kuonekana kwa mwandamo wa mwezi hakukuthubutu kwa mujibu wa masharti ya kisheria, hivyo basi kesho, Jumatatu, inakamilisha mwezi wa Sha'aban, na Jumanne itakuwa ndio siku ya kwanza ya mwezi mtukufu wa Ramadhan ya mwaka 1442 Hijria.

Kwa mnasaba huu, nawasilisha salamu zangu na pongezi za Mkuu wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na wale wote wanaofanya kazi ndani yake, kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah, nikimuomba Mwenyezi Mungu kumnusuru na kuharakisha ushindi kwetu na tamkini kupitia mikono yake.

Ramadhan mwaka huu inatutembelea na huku ulimwengu unaongezeka kuchanganyikiwa na kushughulishwa na majanga. Kushindwa kwa mfumo wa kirasilimali imekuwa ni jambo linaloonekana wazi miongoni mwa ya duara za watawala na watoaji maoni katika miji mikuu ambayo mfumo wa kirasilimali ulianzia. Watu wa nchi za Magharibi wanatazama kwa tashwishi tabia zote za serikali zao, huku nchi zinazokaliwa na Magharibi – kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja - zinatumbukia kwenye majanga, ukosefu wa utulivu na hata ghasia. Na watu wa nchi za Kiislamu haswa wanalipia gharama maradufu kwa kipindi cha miaka mia moja iliyopita, kwa pamoja.

**Gharama ya kwanza ni kuendelea kudhalilishwa kimataifa kwa Umma wa Kiislamu tangu Khilafah ilipo vunjwa.** Ishara ya udhalilishaji huu ilianza wakati Jenerali Gouraud alipolipiga teke kaburi la Salahuddin, Mwenyezi Mungu amrehemu, na sio la tukio la mwisho Ufaransa yaendelea na kumtukana bwana wetu Muhammad (saw). Mwenyezi Mungu (swt) asema:

قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاء مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ

**"Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi."** [Aal-i-Imran: 118].

**Ama gharama ya pili, ni kuishi maisha yaliyojaa migogoro na misiba.** Chini ya utawala wa mfumo wa kirasilimali, nchi nyingi za Kiislamu zimekuwa chini ya mzigo wa migogoro mibaya sana. Hivyo basi migogoro ya kiuchumi, usalama na kijamii imeathiri viwango vya maisha vya mamia ya mamilioni ya Waislamu. Leo, uhamiaji na kukimbia nchi imekuwa mwenendo kwa watu wa Umma wa Kiislamu!

***Endelea... UK 4***

Miaka mia moja iliyopita imethibitisha kuwa mkoloni kafiri Magharibi haitaondoa udhalilishaji na mateso haya kutoka mabegani mwa Umma wa Kiislamu maadamu inadhibiti hatma yake. Mwenyezi (swt) asema:

وَإِن يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ لاَ يَرْقُبُواْ فِيكُمْ إِلاًّ وَلاَ ذِمَّةً

**"… Nao wakikushindeni hawatazami kwenu udugu wala ahadi?"** [At-Tawba: 8].

Kuanzia mateso ya Wauyghur na mauwaji ya Rohingya, hadi uharibifu wa Ash-Sham na ukaliaji wa Al-Aqsa; mwanzo wa mizozo hii yote ilikuwa kupoteza uwezo wa Waislamu kusimamia mambo yao kwa sababu ya kukosekana kwa dola inayowakilisha maslahi haya.

Lakini maumivu haya ya miaka mia moja, pamoja na uwepo wa wabebaji wa Dawah, yameufanya Ummah kutambua, kwa busara na kwa dhahiri, kwamba ulipoteza fahari yake wakati ulipo poteza Khilafah yake, na utambuzi huu uliifanya Khilafah kuwa **ndio rai jumla ya umma miongoni mwa Waislamu, wakiangalia na kutamani kurudi kwake.**

Pia, matokeo ya maumivu hayo, ni kwamba Ummah ilifahamu juu ya kujitiisha kwa watawala wake na kuusaliti kwao. Hamu yao ni kutumikia maslahi ya mkoloni kafiri Magharibi, na wameisaidia kupora utajiri wa Ummah, kuangamiza ardhi zake na kuua watoto wake. Hii iliufanya Umma **utambue kuwa nguvu zake zilinyang'anywa na unahitaji kukombolewa. Leo, watu wake wamekasirika na kulipuka, tayari kutoa damu yao ili kurudisha tena mamlaka yao.**

**Ama kuhusu ubwana wa Shariah,** Umma bado haujaamua juu ya faradhi hii. Tunauona katika hali na matukio mingi ukisita kuufanya ubwana huo kuwa kwa Sharia pekee, kwa hivyo unaleta sheria zengine pamoja na Shariah ya Kiislamu katika suala la utawala. Sababu ya hili ni kukosa ujasiri katika uwezo wa Shariah kutawala maisha, kwa kuongeza kujisikia duni dhidi ya nguvu ya mkoloni kafiri Magharibi.

Hapa inakuja dori ya wale Waislamu ambao wanahusika na mimbari, mabaraza, vikundi, majukwaa na vyombo vya habari, na wale Waislamu ambao Mwenyezi Mungu (swt) amewawezesha kuwa katika nafasi za mamlaka na ulinzi katika Umma wa Kiislamu.

**Enyi Wamiliki wa Mimbari, Majukwaa, Mabaraza na Vikundi … Enyi Waja wa Mwenyezi Mungu:**

Mumekubali jukumu la kuunda rai jumla ya umma, na Mwenyezi Mungu atawauliza juu ya kile alichowakabidhi na hivyo kuufanya Umma kuwa thabiti katika imani yake juu ya sheria ya Kiislamu na uwezo wake wa kusimamia maswala ya maisha ni jukumu lenu, na pia kuufundisha juu ya uharamu wa kuchanganya sheria zengine na sheria ya Mwenyezi Mungu ni jukumu lenu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ

**"Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi."** [Al-Ahzab: 36].

**Enyi Watu wa Nguvu na Ulinzi … Enyi Waja wa Mwenyezi Mungu:**

Tunawasihi, katika mwezi huu mtukufu, mutimize wajibu wenu mliopewa na Mwenyezi Mungu (swt) wa nguvu na ulinzi, na mutekeleze kwa vitendo ili kusimamisha sheria ya Mwenyezi Mungu. Kwa kutoa nusra kwa Hizb ut Tahrir, kiongozi asiyewadanganya watu wake, utawala wa Magharibi utaondolewa kutoka nchi za Kiislamu, na mamlaka ya Ummah yataregeshwa. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

**"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu."** [Muhammad: 7].

Mwezi wenu uwe wenye Baraka, Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh.
Mkesha wa Jumatatu unakamilisha mwezi wa Sha'aban ya mwaka 1442 H.

**Mh. Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Ramadhan: Tuzidisheni Juhudi Katika Ulinganizi wa Kurudisha Khilafah

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



Ramadhan ya 1442 Hijria inatukaribia na ilhali bado Waislamu na wanadamu jumla wamebakia mayatima. Wamezungukwa na majanga ya kila aina yakijumuisha ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kielimu n.k. Watawala wajinga (ruwaybidha) wanaendelea kutawala kwa kutumia ufisadi kwa ushirikiano na wakoloni Wamagharibi. Ufisadi - kujisalimisha kwa itikadi ya kisekula (ilmaniya). Hivyo basi, kusimamia mambo ya watu kwa mujibu wa mfumo wa kirasilimali na nidhamu zake ovu hususan demokrasia.

Nidhamu ya kidemokrasia ndio nguzo muhimu baada ya ile ya kiuchumi katika mfumo wa kirasilimali. Ndio inayowapa wanadamu nguvu za kujitwika jukumu la Mwenyezi Mungu (swt). Jukumu ambalo ni haki ya Muumba wa viumbe (ulimwengu, mwanadamu na uhai), nalo ni utungaji sheria. Badala yake leo wanadamu wanajitungia sheria kwa mujibu wa akili zao zenye kikomo na zisizodiriki dhati ya Mwenyezi Mungu (swt). Wanahalalisha na kuharamisha kwa kutegemea mapenzi ya nafsi zao!

Kupitia utekelezwaji wa mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake, tunaendelea kushuhudia kwa kasi mporomoko na majanga makubwa. Hakuna nyanja hata moja katika maisha imesalimika na jinamizi hilo. Waislamu na wasiokuwa Waislamu wamo katika wasiwasi wa kudumu. Kwa kuongezea kila mmoja anatapatapa kujinasua kwa njia awezayo. Wote wakijifunga na kufirikia ambako kunalirudia sanduku hatari la mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake.

La msingi ni kujua kwamba chanzo cha tabu zote tunazozipata wanadamu hivi leo ni kwa sababu ya kutoizingatia kauli ya Mwenyezi Mungu (swt):

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ أَعْمَىٰ

**"Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu."** [Ta Ha 20: 124].

Baada ya kufahamu hilo tunatakiwa kurudi nyuma na kutathmini tulipokosea na kurekebisha kwa haraka na dharura.
La kusikitisha licha ya kujua mzizi wa matatizo bado wanadamu wamo katika kujipa matumaini feki kwa kutafuta suluhisho ndani ya takataka zilezile ambazo

***Endelea... UK 6***



Email: info@uqab.or.ke

ndio tatizo haswa! Kwani wameweka juhudi katika kupitisha, kubadilisha na kurekebisha katiba na kanuni walizozitunga! Wengine wakiweka juhudi katika kuwaweka au kuwatoa mamlakani viongozi! Lakini hatua zote hizo hazija punguza kasi ya mporomoko na majanga bali kila kukicha ndio kunazidi ukosefu wa usalama, utulivu na ustawi.

Bila shaka kila mwenye akili tambuzi anafahamu kwamba mti wenye sumu utaendelea kuzaa matunda ya sumu. Na hata ukatumia juhudi na nguvu kiasi gani katika kuudhibiti mti huo ikiwemo mfano kukata tagaa au kuyaondosha majani. Kattu mti utaendelea kuzaa matunda ya sumu kwa kuwa mizizi yake ipo! Hatua pekee ni kuung'oa mti huo pamoja na mizizi yake na mahali pake kupandwa mti wenye kuzaa matunda yasiokuwa na sumu. Kupitia mti huo mpya wanadamu watanufaika na kusalimika.

Ramadhan hii itakuwa ni ya 100 pasina kuweko Dola ya Kiislamu, Khilafah ikiongozwa na mtawala, Khalifah. Mtawala anayetumia Qur'an na Sunnah katika kuwasimamia watu mambo yao. Mtawala atakaye kuwa mlinzi, ngao na mtetezi wa Ummah pasina kuzingatia dini, kabila wala rangi za anao watawala.

إِنَّمَا الإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ

**"Imamu (Khalifah) ni ngao kwao. Wanapigana nyuma yake na kujilinda kwake."** [Muslim].

Ni fursa adhimu katika mwezi wenye baraka ambao nafsi za Waislamu zimejaa hamu na shauku ya kupata msamaha kwa madhambi yao kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). Ni mwezi ambao wanaume na wanawake hushindana katika kutafuta kheri za Mwenyezi Mungu (swt). Nafsi huzidi kulainika na kuwa haraka katika kumuitikia Mwenyezi Mungu (swt) Anapowaita waumini. Huu ndio msimu wa kuwavuna wapenda kheri wenye kuipenda Dini yao ya Uislamu hususan katika zama hizi ngumu.

Ulinganizi wa kurudisha maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume ni mchakato adhimu. Hakika unawahitaji wapenda kheri walio tayari kujitoa muhanga kumnusuru Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume (saw). Ili kujiunga na kufanyakazi pamoja ili kuwakomboa wanadamu jumla kutoka katika makucha ya mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake chafu. Tuzidisheni juhudi katika ulinganizi wa kurudisha Khilafah kwani ndio mama wa faradhi zote.

Khilafah pekee ndiyo itakayotuunganisha kuwa Ummah mmoja, Dola moja chini ya Mtawala mmoja. Kuwepo kwake ndipo heshima, hadhi, damu na mali za watu zitahifadhiwa kiukweli. Hatimaye tutapata utulivu, ustawi na maendeleo kutokana na kutekelezwa kwa Qur'an na Sunnah katika nyanja za maisha.


Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI
# BATUK - Zana ya Kikoloni yenye Kulinda Maslahi na Ajenda ya Kikoloni

**Habari:**

Mnamo Jumanne, 6 Aprili 2021, Mkuu wa Majeshi ya Uingereza Jenerali Bwana Nick Carter alizuru Kenya na kumtembelea Mkuu wa Majeshi Jenerali Robert Kibochi katika Makao Makuu ya Jeshi huko Nairobi. Wawili hao walijumuika katika maongezi ya pamoja kuhusiana na ushirikiano baina ya majeshi ya mataifa hayo mawili.

Jumanne mchana, Jenerali Bwana Nick alitoa hotuba kuhusu Mchakato wa Usalama wa Kimataifa katika Chuo cha Ulinzi wa Kitaifa akiwa mwenyeji wake ni Kamanda, Luteni Jenerali Adan Mulata. Hatimaye, mnamo Jumatano, alikamilisha ziara yake kwa kuzuru Kitengo cha Mafunzo cha Jeshi la Uingereza (BATUK) huko Nanyuki ambako alijuzwa kuhusu mafunzo na mazoezi ya kijeshi ya pamoja ambayo wanajeshi wa Uingereza hushiriki wanapokuwa Kenya. (https://mod.go.ke)

**Maoni:**

Bila shaka ziara hii ilikuwa ni ya hatua iliyozingatiwa kwa kina na bwana mkoloni Muingereza ili kuwatuliza mameneja wake vibaraka watiifu. Hii ni baada ya matukio matatu nyeti yanayochipuza kutoka Uingereza. Kwanza – ni tukio la wanajeshi wa Uingereza kuleta nchini Kenya aina ya virusi vya Covid-19 kutoka Uingereza vinavyojulikana kama B.1.1.7 walipokuwa wanakuja kwa mafunzo. Pili – moto mkubwa ulioanza mnamo Jumatano, 24 Machi 2021. Wanajeshi wa Uingereza chini ya BATUK walisababisha moto mkubwa walipokuwa mafunzoni kwa kinachodaiwa kuwa ni kifaa cha ulipuzi kilichoboreshwa. Moto huo ambao ulichukua takribani siku 5 kuuzima, uliharibu zaidi ya ekari 12,000 za Mlima wa Loldaiga.

Hayo yalipelekea shirika la kimazingira, Kituo cha Kiafrika kwa ajili ya Hatua za Kurekebisha na Kuzuia (ACCPA) kulishtaki Jeshi la Uingereza kwa tukio hilo. Kwa kuongezea, ACCPA ilitoa ombi kwa BATUK na Hifadhi ya Loldaiga kuwapa fidia wenyeji walioathirika na madhara ya kimazingira yaliyo sababishwa na moto huo. Tatu – ilani isiyoingia akilini dhidi ya usafiri kwa Kenya iliyotolewa na Uingereza na kuisababisha serikali ya Kenya kulipiza kisasi!

Kenya ni taifa huru katika karatasi lakini ni koloni la Uingereza katika muktadha halisia. Kando na kuwa Kenya ni mwanachama wa Jumuiya ya Madola, imeidhinisha makubaliano yanayoitia minyororo Kenya kwa bwana wake mkoloni. Baadhi ya mikataba hiyo ni Makubaliano ya Ushirikiano wa Kijeshi na Uingereza ambao upo zaidi miaka 40! Katika mpango huo wanajeshi wa Uingereza wanatakiwa kuwepo nchini Kenya kwa ‘sababu za kimafunzo.’

Kwa hiyo, imepelekea zaidi ya wanajeshi 10,000 wa Uingereza kufanya mafunzo nchini Kenya kila mwaka! Kwa maandalizi ya kutumwa katika maeneo yenye anga sawia nayo kama Afghanistan na Iraq. Hivyo basi, BATUK ni kitengo cha kudumu chenye kutoa msaada kilichoko haswa Nanyuki kikiwa na kambi ndogo huko Kahawa. Kwa kuongezea, Uingereza inayo Timu ya Uingereza Yenye Kutoa Msaada kwa Afrika Mashariki (BPST-EA). Lengo lake ni kuratibu msaada wa kijeshi wa Uingereza kwa vikosi vya kijeshi ndani ya Afrika Mashariki kama vile Mafunzo kwa AMISOM Kabla-Kutumwa vitani n.k.

Inafahamika kuwa yeyote anayedhibiti jeshi ndiye anayedhibiti taifa. Kwa kuwa Uingereza inapatiliza mahusiano yake ya kikoloni kwa Kenya na ambayo ushawishi wake unapenya ndani ya safu za muundo wa Jeshi ambao msingi na mawe ya ujenzi wake yamewekwa na yeye. Mwishowe malengo yake ni kulinda maslahi na ajenda yake nchini Kenya na ndani ya eneo pana la Afrika Mashariki. Hivyo basi, vita dhidi ya ‘Ugaidi’ na ‘Misimamo Mikali’ vinatoa fursa ya dharura muhimu ili kuendeleza kasi za mipango ya kijeshi hususan sasa hivi ambapo Uingereza imetoka ndani ya Muungano wa Ulaya (EU).


Uingereza iko mbioni kujiweka vizuri ili kupangilia sera na mbinu zake ili kuweza kunyanyua haiba yake inayodorora ikiwa pweke hivi leo. Kwa hiyo, haya makosa mapya yaliyojitokeza kutoka upande wa Uingereza ni upepo dhaifu vilivyostahiki ziara ya siku mbili kutoka kwa Mkuu wa Majeshi ya Uingereza ili kuwatuliza mameneja katika shamba la kikoloni. Hali itabakia kama ilivyokuwepo awali kama inavyothibitishwa na ukimya wa Wizara za Majeshi na Mazingira kuhusiana na kelele kutokana na uharibifu uliofanyika kwa mazingira. Pia, mzozo wa kidiplomasia utafifia.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



Email: info@uqab.or.ke

# Ramadhan na Ihsan: Kuutafuta Ukamilifu Katika Kumuabudu Mwenyezi Mungu




Mwenyezi Mungu (swt) asema katika Kitabu chake kitukufu:

﴿لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۖ وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ وَلَا ذِلَّةٌ ۚ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ﴾.

**"Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi. Wala vumbi halitawafunika nyuso zao, wala madhila. Hao ndio watu wa Peponi. Humo watadumu."** [Yunus: 26]

Katika Ayah hii nzuri ya Qur'an, Mwenyezi Mungu (swt) anaahidi mambo ya ajabu zaidi ambayo yatalipwa kwa wale wanaofanya mema, na ushindi wake, msaada, utunzaji na tawfiq yake. Malaika Jibril, amani iwe juu yake, wakati mmoja alimuuliza Mtume (saw):

**"فأخبرني عن الإحسان؟..."**

**"Nipe habari kuhusu ihsan"** Mtume akamwambia:

«الْإِحْسَانُ أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ»

**"Ihsan ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba wamuona, basi ikiwa humuoni hakika Yeye yuakuona"** (Bukhari na Muslim). Wanachuoni wameifafanua ihsan kuwa ni kujitahidi kwa ukamilifu, ikhlasi na ubora katika kumtii Mwenyezi Mungu.

Mwezi wa Ramadhan ni wakati mwafaka kwetu kuelewa na kufikiria juu ya mada hii muhimu. Katika mwezi huu uliobarikiwa, tunajaribu kujadidisha uhusiano wetu na Mwenyezi Mungu na kuleta mabadiliko bora kwa maisha yetu na kwa ajili ya maisha yetu ya duniani na Akhera yetu. Kwa hivyo, kipindi hiki cha siku hizi zenye baraka, sisi katika Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir, tunataraji kuangazia maswala haya kwa upana katika maudhui yetu ya: **"Ramadhan na Ihsan."**

**Dkt. Nazreen Nawaz**

**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**




Email: info@uqab.or.ke

# JIBU LA SWALI

# Tofauti ya Rai za Kifiqhi

## Kwa Mfano Kuthubutu Kuanza kwa Kufunga Ramadhan




**Swali:**

Assalam Aleykum wa Rahmatullah wa Barakatuh

Swali kwa Emir wetu na Sheikh wetu, Amiri wa Hizb ut-Tahrir, Sheikh Ataa bin Khalil Abu Al-Rashta, Mungu amhifadhi, na aujaaliye ushindi wa Uislamu na utukufu wake mikononi mwake na mikononi mwa kundi la waumini miongoni mwa Mashababu wa Hizb ut-Tahrir pamoja naye.

Sheikh wetu mkubwa, nina swali juu ya rai za kifiqhi za maimamu wanne na mujtahidi wengine ambao wanatofautiana na sisi kuhusu rai za kifiqhi zilizo tabanniwa katika Hizb, na ambazo zinaingia katika ile inayoitwa fiqhi ya ikhtilaf. Mfano: Kuthubutu mfungo wa Ramadhan kupitia hesabu ya falaki, na ambayo baadhi ya mafuqaha (wanachouni wa fiqh) wa zamani, kama Ibn Sarij al-Shafi'i na wengineo miongoni mwa mafuqaha, kama Sheikh Ahmed Shaker al-Masri na Sheikh Mustafa al-Zarqa al-Halabi al-Hanafi, walisema kwa kina rai yake kwa vile ninavyo dhani mimi. Swali ni: Je! Tutaamiliana vipi na rai hizi zinazo tofautiana na zile tulizozitabanni katika Hizb, haswa ikiwa ni za maimamu mujtahidina wakubwa? Kwa mfano, je! Tukubali suala la kuthubutu kufunga kwa njia ya hesabu ya falaki, kwamba katika suala hili kuna rai mbili na kwamba rai ya wengi ni kwamba inaruhusiwa na sio lazima, na tukubali kauli ya yule mwenye kusema "Usinilazimishe katika suala ambalo kuna ikhtilafu baina ya wanachuoni wa fiqh; rai yoyote ninayoifuata mimi kati ya hizo ni sawa"?

Kusudi la swali hili ni kutilia nguvu ufahamu wangu wa fiqhi ya ikhtilaf, na ni wakati gani rai ya pili inakuwa na nguvu, kwa mfano, na ni wakati gani rai ya pili inakuwa ni yenye kukataliwa na kupaswa kupigwa vita, na ni wakati gani, kwa mfano, rai ya pili inakubali ikhtilafu hata kama ni yenye nguvu kwa mtazamo wetu? Kwa mfano: Je! Kuna tofauti gani kati ya suala la kuthubutu kufunga Ramadhan kwa hesabu ya falaki katika upande wa kukubali rai ya nyengine na baina mfano uchi wa mwanamke kuhusiana na mwanamume yenye kuhitilafiana na rai ya Hizb ambayo inasema kuwa uso na mikono ni uchi ?

Naomba radhi kwa kurefusha. Lakini natarajia ufafanuzi wa ni kwa nini mtazamo ume tofautiana, kwa kweli kwa mtazamo wangu, "na naomba radhi ikiwa nimekosea"?

***Endelea... UK 10***


Email: info@uqab.or.ke

Je! Sababu ni ukaribu na umbali wa hukmu hizi kutoka kwa umoja wa Khilafah na kuungananisha mtazamo kwake, au ni kitu kingine?

Mwenyezi Mungu awalipe kheri, Wassalamu aleykum wa Rahmatullahi wa Barakatuh.

**Jibu:**

Wa aleykum Salaam wa Rahmatullah wa Barakatuh,

Mwenyezi Mungu akubariki kwa dua yako nzuri kwetu nasi tunakurudishia dua ya kheri na baraka…

Hakika hukmu ambayo imevuliwa kutokana na dalili za kisheria kupitia ijtihad sahihi ya kisheria ni hukmu ya kisheria katika haki ya mmiliki wake, na ni rai ya Kiislamu hata ikiwa inatofautiana na rai tunayoisema na rai tunayoitabanni, haswa ikiwa rai hii ni rai ya mujtahid miongoni mwa maimamu wa madhehebu mashuhuri kwa elimu na ucha Mungu, kama vile ijtihad za maimamu wa madhehebu manne na mujtahidina wa madhehebu hayo ... Na tumebainisha jinsi ya kuamiliana na rai za kifiqhi ambazo zinatofautiana na rai za kifiqhi tulizozitabanni katika zaidi ya kitabu kimoja miongoni mwa vitabu vya thaqafa ya Hizb, na nakunukulia kutoka katika sehemu mbili yale ambayo yatafaa kuwa ni jibu la swali lako, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu:

**1- Katika kitabu cha "Mafahim ya Hizb ut-Tahrir" yamekuja yafuatayo:** [Na kuamini Uislamu ni kando na kuzifahamu hukmu na sheria zake, kwa sababu kuuamini kumethubutu kupitia njia ya kiakili, au kwa njia ambayo asili yake imethubutu kiakili, na kwa hivyo hakuna nafasi ya shaka kwa hilo. Ama kuhusu kuelewa hukmu zake, haimalizikii na akili peke yake, bali inategemea ujuzi wa lugha ya Kiarabu na uwepo wa uwezo wa kufanya uvuaji, na maarifa ya hadith sahihi kutoka kwa dhaifu. **Kwa hivyo, wabebaji wa da'wah wanapaswa kuuchukulia uelewa wao wa hukmu kama uelewa sahihi unaoweza kuwa na makosa, na wauchukulie uelewa wa wengine kuwa ni wa makosa unaoweza kuwa sawa, ili waweze kuulingania Uislamu na hukmu zake kulingana na uelewa wao na uvuaji wao kwake, na kuhamisha uelewa wa wengine ambao wanauchukulia kuwa wa makosa na wenye uwezekano wa kuwa sawa hadi katika uelewa wao ambao wanauchukulia kuwa sahihi wenye uwezekano wa kuwa na makosa. Kwa hivyo, sio sahihi kwa walinganizi wa da'wah kusema kuhusu uelewa wao, kwamba hii ndio rai ya Uislamu. Badala yake, wanapaswa kusema kuhusu rai yao, kwamba hii ni rai ya Kiislamu. Watu wa madhehenu miongoni mwa mujtahidina wanauchukulia uvuaji wao wa hukmu kuwa sahihi na wenye uwezekano wa kuwa na makosa. Na kila mmoja wao anasema: "Pindi inapo swihi hadith basi ndio madhehebu yangu, kisha yapigeni maneno yangu ukutani". Vivyo hivyo, wabebaji da'wah wanapaswa wazingatie rai zao wanazozitabanni, au wanazozifikia kutoka katika Uislamu, kwa kuzingatia uelewa wao, kuwa ni rai sahihi zenye uwezo wa kuwa na makosa.]** Mwisho.

2- Na imekuja katika kjiitabu cha Kuingia kwa Jamii yafuatayo: [... Ama kwa upande wa kuingia, inapaswa kutoruhusiwa isipokuwa kuingia kwa Uislamu peke yake, bila kasoro zote, kwani makafiri, watawala na wanasiasa watajaribu kuingiza fikra zisizokuwa za Kiislamu kwa jamii chini ya jina la Uislamu, ili waweze kutia shaka katika jamii kwa upande wa Uislamu, kwa hivyo Waislamu lazima wawe juu ya utambuzi kamili katika upande huu. Kwa hivyo washambulie fikra yoyote inayo halifiana na Uislamu kama ambavyo wanapaswa kushambulia fikra yoyote ya ukafiri, kwa sababu ni ukafiri ulio wazi.

Isipokuwa, kwamba shambulizi hili liko tu kwa fikra za kisiasa au za kisheria, yaani juu ya fikra zinazohusiana na mahusiano ya jamii ambayo yanajadiliwa katika maswala ya dola wakati fikra inapotolewa au wakati utafiti unapofanywa. Na mfano wa hilo, ni marufuku ya kuoa wake wengi, kuhalalisha vyama vya misaada, ushiriki katika wizara, kujikaribisha kati ya watawala wa dola zilizopo katika ulimwengu wa Kiislamu katika kulinda kubakia kwa kila mtawala kama alivyo, Chuo Kikuu cha Kiislamu, kuinua kiwango cha maisha, kuingiza pesa za kigeni katika nchi, na kadhalika. Hizi zote ni fikra zisizo za Kiislamu ambazo huja kwa kisingizio kwamba ni za Kiislamu, au kwamba hazipingani na Uislamu. Hizi lazima zishambuliwe na kupigwa vita na zisiweze kuingia katika jamii ili kusitokee tashwishi ndani yake. **Ama fikra za Kiislamu ambazo zinatofautiana na kile ilicho tabanni Hizb, hubainishwa makosa ya uelewa kwake, lakini hazishambuliwi, badala yake huwekwa wazi kuwa ni rai ya Kiislamu, lakini dalili yake ni dhaifu. Kwa mfano, miongoni mwa mujtahidina ni wale wasioruhusu khalifa isipokuwa Mquraishi pekee au kutoka kwa familia ya Mtume (aali bait), na wengine wao wanaona kuwa haikubaliki kwa mwanamke kuwa qadhi, na wengine wao wanaona kuwa inaruhusiwa kulimbikiza dhahabu na fedha ikiwa zaka yake inalipwa, na wengine wanaona kuwa inaruhusiwa kukodisha ardhi kwa ajili ya kilimo, na kadhalika. Rai hizi zote ni rai za Kiislamu na hazizuiwi kuingia katika jamii kwa sababu hakutokei ndani yake tashwishi kwa sababu ni za Uislamu kama rai zilizotabanniwa na Hizb, zinatokana na dalili au dalili madhaniwa. Inatosheleza kuhusiana na fikra hizi za Kiislamu, kuelezea tu makosa yake.**

Isipokuwa kwamba Hizb katika magazeti yake, taarifa zake na majadiliano yake kamwe haibebi rai yoyote inayo tofautiana na yale iliyoyatabanni, lakini inaruhusiwa kusambaza rai ambazo haijazitabanni kama mifano ya ufahamu wa kifiqhi au wa kisheria, bila ya kunasibishwa na wale walioitoa, bali inatosheleza dalili yake. Hii ni kwa upande wa rai ambazo Hizb inazisambaza, ama inaposambazwa rai ya Kiislamu, kwa njia isiyokuwa ya Hizb, na ikawa rai hii inagongana na rai ya Hizb,

*Endelea... UK 11*

basi inatosheleza kuijadili ikiwa kuna haja ya kuijadili, vinginevyo itapuuzwa. Katika haya yote, Hizb inazunguka kati ya jamii na tashwishi ambayo inaogopa isitokee ndani yake. Vita vitaendelea kati ya Uislamu na ukafiri hadi ukafiri utakaposhindwa na Uislamu ushinde.] Mwisho.

Ni wazi kutokana na kile kilichonukuliwa hapo juu kwamba Hizb haikatai kwa wengine kauli ya rai za kifiqhi ambazo zinatofautiana na yale iliyoyatabanni maadamu zimevuliwa kwa ijtihad sahihi ya kisheria, na ikiwa jambo liko hivi basi hailikatai kwao, lakini badala yake inajadiliana nao na kujaribu kuwakinaisha juu ya makosa ya rai zao na usahihi wa rai zake kwa msingi wa dalili, wala haizipigi vita rai zao wala haizishambulii, lakini inatosheka na kuelezea makosa ndani yake, na inaruhusu kuwepo kwake katika jamii kwa sababu ni rai za Kiislamu hata kama zina dosari na udhaifu katika dalili kwa upande wa Hizb...

- Na katika mifano ya hilo ni kauli kwamba uso wa mwanamke na mikono ni uchi, ni rai ya kifiqhi ya Kiislamu ambayo baadhi ya wanachuoni wa kifiqhi na mujtahidina wameizungumza, na hatuwapingi wale wanaoisema, lakini tunawaita kwenye rai yetu isemayo kwamba uso wa mwanamke na mikono sio 'awrah, na tunawabainisha kwa dalili za Kisheria usahihi wa rai yetu, lakini hatuzishambulii rai zao hizi, wala hatuwapingi wafuasi wake kwa sababu ni rai za Kiislamu zilizosemwa na wanachuoni wa kifiqhi ambao ni mujtahidina...

- Ama kauli ya hesabu za falaki, ina kauli nyingi kwa mujibu wa wale wanaoisema ... Miongoni mwao wanaona kuwa mwezi mwandamo ikiwa utachomoza usiku, basi usiku huo ni wa kwanza wa Ramadhan ... na wengine wao wanasema kwamba ikiwa mwezi mwandamo utachomoza wakati wa mchana na kupotea baada ya kutua kwa jua bila kujali muda wa kupotea, usiku huu ni wa Ramadhan ... na wengine wao hujaribu kupatanisha kati ya hesabu na kuonekana, na kusema kwamba ikiwa utachomoza wakati wa mchana na kupotea baada ya jua kuchwa kwa kipindi ambacho inawezekana kuuona, basi usiku huo utakuwa ni wa kwanza wa Ramadhan ... kisha wanatofautiana katika kiwango cha muda huu, je ni dakika 10, 15 au 20, na kadhalika ... na mimi siegemei mwelekeo wa kuwa hii ni ijtihad sahihi. Maandiko yako wazi yakiunganisha kufunga na kufungua saumu kwa kuonekana,

صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ

**"Fungeni kuonekana kwake, na fungueni kwa kuonekana kwake."**

Imepokewa na Muslim, kwa hivyo vipi wanageuza hili kwenda kwenye hesabu? Haswa Mtume (saw) Haswa kwa kuwa Mtume (saw) alijaaliya ukosefu wa kuonekana kwa sababu ya mawingu kwa mfano, hata ikiwa mwezi mwandamo uko nyuma ya mawingu, lakini mawingu yanauficha usionekane. Alijaaliya ukosefu wa kuonekana katika hali hii kuwajibisha kukamilisha Shaaban siku 30 hata kama mwezi mwandamo ulikuwa nyuma ya mawingu lakini haukuonekana.

فَإِنْ غُمِّيَ عَلَيْكُمُ الشَّهْرُ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ

"Ikiwa kwenu mwezi utazibwa na mawingu, basi hesabuni thalathini" Imepokewa na Muslim, na yote haya yanathibitisha kuwa sababu ya kufunga na kufungua ni muonekano na sio sababu nyingine yoyote. Kwa hivyo, katika nafsi yangu nina kitu kwamba hesabu ya falaki haikuvuliwa kwa ijtihadi sahihi ya kisheria ... Sisi tumetabanni muonekano wa kisheria kwa sababu umejengwa juu ya ijtihad sahihi ya kisheria kwa mujibu wa misingi sahihi ya kisheria, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

- Kwa kumalizia, sisi hatushambulii rai yoyote ya Kiislamu iliyosemwa na mujtahidina waheshimika maadamu imevuliwa kutoka kwa Uislamu kwa ijtihad ya kisheria, lakini badala yake tunajadiliana nao kwa uzuri kwa kuwa rai yetu ndio sahihi na tunazitaja dalili na kusikia kutoka wao ... Lakini tunasimama kidete mbele ya wale wanaotaka kuingiza rai yasizo za Kiislamu na kupotosha watu kwazo ambazo ziko mbali na Uislamu umbali wa Mashariki mbili! Rai hizi sio sahihi katika kuelezea uongo wao, kama vile kusema kwamba faida za riba zinaruhusiwa, na kusema kwamba inaruhusiwa kushiriki katika nidhamu za kikafiri na kutawala kwa yasiyo kuwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, mpaka hali hiyo imewafikisha kusema kwamba maridhiano (amani) na Mayahudi na kusawazisha mahusiano na umbile hilo lao inaruhusiwa ﴿أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ﴾ **"Tazama uovu wa wanavyohukumu!"** na mfano wa hizo katika rai ambazo zimeenea katika zama zetu na ambazo hazikuvuliwa uvuaji sahihi wa kisheria. Badala yake, baadhi yake zinapingana na dalili za kukatikiwa kutoka kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume (saw), kwa hivyo mfano wa rai kama hizi hazizingatiwi kuwa ni hukmu za kisheria wala kuwa ni rai za Kiislamu, na hupingwa wale wanaozisema na kuzibeba, na kuzipiga vita na kuzuiwa uwepo wake ...

Nataraji kuwa hii imetolesheleza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi Mwingi wa Hekima.

**Ndugu yenu,**

**Ata bin Khalil Abu Al-Rashtah**

# DHULMA NA UONEVU WALIOFANYIWA, INATOSHA



**Ust. Ramadhan Moshi Kakoso**
**Mwalimu wa dini ya Kiislamu na mfanyabiashara**

Tarehe 30/10/2017 Ustadh Ramadhan Moshi KakosoAlitiwa nguvuni Nyumbani kwake Magomeni Makuti, Dar es Salaam mbele ya familia yake na watu waliojitambulisha kuwa maafisa wa usalama. Baada ya shinikizo la Ustadh Rashid Moshi Kakoso kwa watu hao waliomtia nguvuni, kwamba kuna ulazima wa suala lake kuarifiwa Mwenyekiti wake wa mtaa, wakapita karibu na Afisi ya Mwenyekiti wa serikali ya mtaa, ambapo maafisa hao waliahidi mbele ya mwenyekiti huyo wa mtaa kwamba taarifa zake zingepatikana katika kituo cha Polisi cha karibu. Tokea alipokamatwa mpaka sasa yupo gereza la Lilungu Mtwara na hakuna Ushahidi uliopatikana. Kesi haisikilizwi, upelelezi haukamiliki.




**Omar Salum Bumbo**
**Fundi mjenzi/ Mwashi**

Tarehe 27/10/2017 Omar Salum Bumbo alinyakuliwa na kutekwa na waoaminika kuwa ni maafisa wa usalama, baada ya mmoja wa maafisa hao kijanja kumpigia simu kwamba angetaka kumpatia Omar Salum Bumbo kazi ya ujenzi, kisha alipofika eneo aliloahidiwa kukutana nae maeneo ya Tabata alitekwa na wanaoaminika kuwa maafisa wa usalama, kumsweka garini, kutoweka nae kusikojulikana, sambamba na kumtisha dereva wa bodaboda aliyemfikisha eneo hilo, kuondoka mara moja. Tokea alipokamatwa mpaka sasa yuko gereza la Lilungu Mtwara na hakuna Ushahidi uliopatikana. Kesi haisikilizwi, upelelezi haukamiliki.



**Suleiman Mkaliaganda**
**Mwalimu sekondari Mtwara mjini**

Tarehe 21/10/2017 Waziri Suleiman Mkaliaganda alinyakuliwa karibu na nyumbani kwake mtaa wa Kiyangu Mtwara mjini. Tokea alipokamatwa mpaka sasa yupo gereza la Lilungu Mtwara na hakuna Ushahidi uliopatikana. Kesi haisikilizwi, upelelezi haukamiliki. Wamerundikwa katika mahabusu zenye mazingara duni kibinadamu, yakikosa usalama wa kiafya na huduma stahiki kwa jumla.

## “waachiliwe Huru”